



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Novemba 15, 2022

## TAARIFA KWA UMMA

Ikiwa ni siku ya pili tangu wanafunzi wa kidato cha Nne kote nchini waanze kufanya Mitihani ya kumaliza Elimu ya Sekondari ambapo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa inatarajiwa kukamilika tarehe 30, Novemba 2022 wanafunzi wote wanaendelea na ufanyaji wa Mitihani hiyo.

Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa inajumla ya shule za Sekondari **23** ambapo shule za Sekondari za Serikali **17** na shule binafsi **6** na jumla ya wanafunzi wanaofanya mtihani huu ni **1,564** kati ya hao wavulana wapo **713** na wasichana **851**.

Aidha watahiniwa wa kujitegemea (PC) wavulana wapo **15** wasichana wapo **24** jumla yao ni **39** na watahiniwa wa Maarifa (QT) ni **19** kati yao wavulana **13** na wasichana **6**.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Nd. Sunday Deogratias anawatakia kila la kheri Wanafunzi wote katika Mitihani hiyo

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.**